Ukambi

Kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Ukambi kwa kutumia chanjo ya MMR

Kwa muda wa miaka kumi iliyopita, Idadi ya watoto wanaopata ukambi nchini Uingereza ilikuwa ya kiwango cha juu sana. Ili kuwa na kinga, mtoto anahitaji dozi mbili za chanjo ya MMR. Watoto wa umri wowote ambao hawajapata chanjo ya MMR wanaweza kupata chanjo ili wapate kinga dhidi ya kupata ukambi.

Kwa nini ukambi unaongezeka?

Katika miaka ya 1990 kuenea kwa ungojwa wa ukambi nchini Uingereza kulizuiliwa kwa sababu ya idadi kubwa sana ya watoto waliopata chajo ya MMR. Tangu 1998 madai ya idadi ndogo ya watafiti kuhusu usalama wa chanjo yalipata nafasi kubwa sana katika vyombo mabalimbali vya kutangaza habari. Ijapoluwa madai hayo yamekanushwa kabisa, watoto wa wazazi wengi ambao waliamua kugomea chanjo ya MMR wakati huu wangali hawajapata chanjo. Idadi ya watoto ambao hawajaanza shule ambao wamesha pata chanjo iko karibu sana na viwango vya juu vilivyopatikana kati ya miaka 1990. Walakini, imekadiriwa kwamba takriban watoto 80,000 wa shule nchini Welisi walikosa dozi moja au zote mbili za MMR. Ni kati ya makundi hayo ya watoto ambako ugonjwa wa ukambi unasambaa kwa urahisi.

Je, ukambi ni ugonjwa mahututi?

Ndio, ukambi unaweza kuwa mahututi na unasababishwa na virusi vinayoambukiza sana. Karibu kila mtu anayepata ukambi ataugua akiwa na homa kali pamoja na vipele. Kwa wastani, mtoto aliye na ukambi atapaswa kulala kama siku tano kitandani na anaweza kukosa kwenda shuleni kwa siku kumi. Watu wazima watakuwa wagonjwa kwa mda mrefu zaidi.

Takriban mtu mmoja kwa watu 15 walio na ukambi watapata madhara mengine amayo yanaweza kuwa ya mahututi.. Haya yanaweza kuwa kama vile, maambukizo ya kuharisha, matatizo ya masikio, kichomi (chest infection), kifafa, maambukizo ya ubongo (uwasho/ kuvimba kwa ubongo), na kuharibika kwa ubongo. Ukambi inaweza kuua na kila mwaka watoto 200,000 ulimweguni wanafariki kutokana na ukambi.

Je, mtoto wangu anaweza kufariki kutokana na ukambi?

Utafiti unaonyesha kwamba kwa kila watu 1,000 wanaopata ukambi, mtu mmoja hadi watu watatu wanaweza kufa kutokana na maambukizo hayo au madhara yanayoambatana nao.

Vijana wawili wamefariki kutokana na ukambi nchini Uingereza miaka michache iliyopita. Mmoja wa umri wa miaka 13 katika mwaka wa 2006 na mwingine wa umri wa miaka 17 katika mwezi wa Juni 2008 – wote wawili walikua na matatizo ya kinga mwili zao kwa hivyo walikuwa hawajapata chanjo ya MMR.

Idadi kubwa ya umma ikipata chanjo, watoto kama hao na wengine ambao wako kwenye hatari ya kuambulizwa ukambi wataweza kukingwa bora ili wasipate ukambi, Matumbwitumbwi na Ukambi wa kijerumani (Rubella).

Je, mtoto wangu yuko hatarini?

Ukambi ni mojawapo ya maradhi yanayojulikana kwa kuambukiza. Kukohoa au kuchafya kunaweza kueneza virusi vya ukambi kwa eneo kubwa. Kwa sababu inaambukiza sana, mtoto wako atakuwa yuko hatarini maishani mwake kupata ukambi kama hajapata chanjo.

Hatari kubwa sana ni kwa watoto ambao hawajapata chanjo ya MMR. Watoto ambao wameshapata chanjo moja pekee wanapaswa kupata dozi ya pili ya chanjo ili wakamilishe chanjo na kuhakikisha ya kwamba wamekingwa kikamilifu. Baadhi ya watoto hawawezi kupata MMR kutokana na hali inayodhoofisha kinga mwili zao, kama saratani ya chembe nyeupe za damu (leukaemia). Watoto hawa wanaweza kukingwa ikiwa watoto wengi walio na afya njema watapata chanjo ili kusambaa kwa Ukambi kuzuiliwe.

Je ninafaa nifanye nini?

Njia salama na imara kabisa ya kukinga ukambi ni kuhakikisha kwamba mtoto wako amepata kikamilifu chanjo ya MMR. Mtoto wako anapaswa kuchanjwa akiwa na umri wa miezi 13 na akiwa na umri wa miaka mitatu na miezi minne au punde baadaye. Ikiwa mtoto wako amekosa chanjo moja (au zote mbili), unapaswa kuzungumza na daktari wako ili akueleze lini utaleta mtoto wako kupata chanjo.

Ni muhimu sana mtoto wako akamilishe chanjo za MMR na apate chanjo mbili. Kuchelewa hakuwezi kuzuia mtoto wako kupewa chanjo.

Sikumbuki ikiwa mtoto wangu amepata au hajapata chanjo ya MMR

Angalia kwa kitabu cha afya ya mtoto wako (Kitabu Chekundu). Kitabu hicho chaweza kuwa na maandishi ya chanjo ambazo mtoto wako amepewa. Ikiwa ungali na mashaka, zungumza na Mhudumu wa afya wako (GP practice) ili akupe mawaidha.

Ikiwa kuna mashaka ni bora kumpa chanjo. Dozi ya zaidi haileti madhara makubwa kwa afya ya mtoto wako ikiwa ameshapata chanjo moja au mbili za MMR.

Mtoto wangu amepata chanjo moja ya ukambi, Matumbwitumbwi na ukambi wa kijerumani (Rubella), je anaweza kupewa MMR?

Ndiyo, ikiwa mtoto hajapewa chanjo ya kumkinga hata mojawapo ya magonjwa hayo, tunashauri apewe dozi mbili za MMR. Kama Wazazi hawana uhakika kwamba mtoto wao amepata kinga kamili kwa chanjo moja, mtoto huyo angali anaweza kupewa MMR. Ni salama mtoto wako kupewa dozi mbili za MMR hata kama amepata chanjo fulani za dozi moja. Unaweza kuzungumza na daktari wako, mgeni wa afya au mhudumu wa afya

Ningali sina uhakika kuhusu kumpa mtoto wangu chanjo tatu kwa sindano moja

Kinga mwili za mtoto zimeundwa kukubali kwa aina tofauti ya vimelea viharibifu (germs) na maambukizo toka kuzaliwa na kuendelea. Kukubali chanjo kunatumia sehemu ndogo sana ya uwezo huo wa kupambana na kitu kinachosumbua kinga - hata kutambaa kwenye sakafu safi ni changamoto kumbwa sana kwenye kinga mwili wao kuliko chanjo kama vile MMR.

Kupata dozi mbili za chanjo ya MMR kutalinda mtoto wako dhidi ya magonjwa yale matatu ya ukambi, matumbwitumbwi na rubella. Magonjwa haya yote matatu yanaweza kuleta madhara makubwa kwa vijana.

Je, chanjo ya MMR ina madhara yeyote?

Chanjo zote zinaweza kuwa na madhara madogo , kama vile maumivu sehemu aliyodungwa sindano. Vile virusi vitatu vilivyomo katika chanjo ya MMR vinafanya kazi kwa wakati tofauti na vyaweza kuleta madhara yafuatayo baada ya dozi ya kwanza:

- Siku sita hadi kumi na mmoja baada ya chanjo, karibu mmoja katika watoto kumi wanaweza kupata joto la mwili lisilo kali na wengine hupata vipelepele vinavyofanana na vya ukambi, na pia watopoteza hamu ya kula..hufanyika hivi wakati virusi vinavyokinga ukambi vinaanza kufanya kazi. kwa ujumla vinadumu siku mbili au tatu;

- Takriban mtoto mmoja kati ya kila watoto 1000 wanaochanjwa anaweza kushikwa na kifafa kinachosababishwa na homa ya mwili. Hii hujulikana kama ‘mitukutiko ya homa’, na huambana na homa kwa sababu tofauti siyo chanjo tu. Walakini, mtoto ambaye hajakingwa akipatwa na ukambi, ana uwezekano mara tano ya kushikwa na kifafa.

- Kwa nadra sana, watoto wanaweza kupata dalili zinazofanana na za matumbwitumbwi, (homa na tezi) takriban wiki tatu baada ya kichanjwa,wakati sehemu ya matumbwitumbwi ya chanjo inapoanza kufanya kazi.

- Kwa nadra sana , watoto wanaweza kupata vipelepele vidogo vinavyofanana na vidoa kati ya wiki sita baada ya chanjo. Kwa kawaida, hivi hujiponesha. Ukiona madoadoa kama hayo, mpeleke mtoto wako kwa daktari kwa ukaguzi. Atakueleza jinsi ya kuvikabili ; na

- chini ya mtoto mmoja katika milioni ndio hupatwa na encephalitis (uvimbe wa ubongo) baada ya chanjo ya MMR, na kuna ushahidi mdogo sana kuwa unasababishwa na chanjo. Walakini, mtoto akipatwa na ukambi, uwezekano wa kupatwa na encephalitis ni kati ya mmoja kati ya 200 na mmoja kati ya 5000.

Daktari wako, mhudumu wa afya au mgeni wa afya ataweza kukushauri zaidi kuhusu swala hili kwa undani.

Je kuhusu mitukio ya baada ya chanjo ya MMR ya pili?

Matukio yaliyotajwa hapa juu yanaweza kutukia, lakini ni kwa nadra sana yatokee..

Ningali na wasiwasi kwamba MMR inaweza kusababisha ugonjwa wa akili ya watoto (autism)

Chanjo ya MMR imeshatumiwa sana na kwa salama duniani kote kwa muda wa zaidi miaka 30. Zaidi ya dozi million 500 zimepatiwa watoto walio katika nchi 100. Utafiti asilia uluiopendekeza kiungo umeshakanushwa kabisa. Utafiti zaidi umefanywa kwa madhumuni ya kupeleleza kiungo kilichopendekezwa na sasa kuna hakikisho kubwa mno kwamba MMR haisababishi ugonjwa wa akili ya watoto (autism). MMR ni salama kama chanjo zinginezo za kawaida tunazozipa watoto wetu ili ziwakinge kutokana na magonjwa hatari ya kuambukiza.

Mtoto wangu ana mizio ya mayai – je, anaweza kupata chanjo ya MMR?

Chanjo ya MMR ni salama kupewa watoto ambao wana mizio ya mayai (athari ya anaphylactic). Kama una hoja zozote, zungumza na muuguzi wa afya, mgeni wa afya, au daktari wako.

MMR ndio njia salama kabisa ya kumkinga mtoto wako dhidi ya ukambi, matumbwitumbwi na rubella.

Je Naweza kupata habari zaidi wapi?

Unaweza zungumza na daktari, mgeni wa afya, au mwuguzi wako, au piga simu
NHS Direct Wales kwa nambari 0845 46 47.

Tazama: **www.mmrthefacts.nhs.uk na**
www.immunisation.nhs.uk
(ili upate habari kinaganaga kuhusu chanjo ya MMR yenye ukambi.)

Kijitabu hiki kinapatikana kwente tovuti ya Welsh Assembly Government immunisation:
http://new.wales.gov.uk/topics/health/
protection/immunisation/leaflets/?lang=en

na katika lugha zifuatazo:

Kiarabu
Kibengali
Kibulgaria
Kichina
Kicheki
Kifarsi
Kifaransa
Kigujerati
Kihindi
Kikurdi (Sorani)
Lingala
Kipolandi
Kireno
Kipunjabi
Kirusi
Kisomali
Kihispania
Kiingereza
Kitagalog
Kiurdu (Naskh)
Kivietnamu

Nakala zinginezo za kijitabu hiki zinapatikana katika Welsh Assembly Government Publications Centre kwa barua pepe:

assembly-publications@wales.gsi.gov.uk

au kwa simu kwa nambari 029 2082 3683 (kati ya 08.00 na 17.00 Jumatatu – Ijumaa)

Maswali yeyote kuhusu kijitabu hiki yanaweza kuulizwa kwenye:

Health Protection Division
Welsh Assembly Government
Cathays Park
Cardiff
CF10 3NQ

Tel:
029 2082 5397 au
029 2082 5410